TANGAZO LA SERIKALI NA.153 la tarehe 3/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA 355)

# AMRI

*(ImetengenezwaChiniyaKifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA ITOLOLO YA MWAKA, 2023.

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Itololo ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura (355)

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa.

*Tangazo la Serikali na.153 (linaendelea)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*
Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VD030 yenye majira – nukta 223012.447MS, 9219583.037KZ; baadayahapompakaunaelekeaKaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ50$^{0}$45'50.00''MS kwa umbali wa kilomita 6.49 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KN2 yenye majira – nukta 228125.090MS,921507.898KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi kwa kufuata ukingo wa mto la Mtera katik auelekeo wa KS23$^{0}$30'53.27''MG kwa umbali wa Kilomita 6.34 hadi kwenye alama ya upimaji namba ya KN3 yenye majira – nukta 225573.014MS, 9209542.668KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi kukatizamto Mloa katika uelekeo wa KS23$^{0}$08'00.21''MG kwa umbali wa kilomita 4.31 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ya KN4 yenye majira – nukta 223875.888 MS, 9205570.229 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki kwa kufuata ukingo wa mto Mloa katika uelekeo wa KS7$^{0}$28'53.30''MS kwa umbali wa kilomita 5.32 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ya KN5 yenye majira - nukta224568.525MS, 9200295.188 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS49$^{0}$14'28.09''MS kwa umbeli wa kilomita 1.04 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ya KN6 yenye majira – nukta 223776.219 MS, 9199612.193KZ; baada ya hapo mpaka unaeleke aKusini-Magharibi katika uelekeo wa KS50$^{0}$43'14.45''MG kwa umbali wa kilomita 3.51 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ya KN7 yenye majira – nukta 221054.704MS,9201838.087 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharib ikatik auelekeo wa KZ3$^{0}$04'51.63''MG kwa umbali wa kilomita 16.03 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba ya KN8 yenye majira - nukta220192.703MS, 9217852.794KZ; baadayahapompakaunaelekeaKaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ58$^{0}$27'57.65''MS kwa umbali wa kilomita3.18 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*